

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam
14 Machi 2009**

Waliohudhuria

Ally Saidi Mwishehe
Bashiri Rashidi
Beda John Mkusu
Edgar R Paulo
Elaine Baker
Filbert Mbecha
Hamadi Hatibu Bwaja
Juma Ali Salehe Jongo
Kibwana Mohammad Msiga
Mohammed Samwely
Mussa Omari
Rahma Ali
Rashidi Saidi Karanji
Shamte J Kigoma
Shukuru Hassan
Sudi Saidi Ramadhan

Mkutano na serikali ya jiji na kongamano

Elaine aliwasiliana zaidi na Bwana Japhet kwa simu. Alisema tukutane wiki ijayo na atatumia siku gani. Elaine atatumia message kwa wanachama wengine atakapopata taarifa.

Mradi wa Wamba

Elaine alichapa repoti na mahesabu Mohammed alizoandika kuhusu mafunzo ya Kigamboni. Ataweka repoti kwenye website.

Helmets 5 na reflective jackets 8 zimebaki. Tulikubali kubaki nazo kwa mafunzo yanayokuja.

Edgar alifuatalia na benki kuhusu hela ya Wamba. Benki wanasema hela haijafika. Elaine alitumia email kwa Una Osili kumwambia na kumwomba afuatalie upande wake kama hela zimekwenda.

Tulianza kuzungumza kuhusu semina kwa waalimu wa udereva kuhusu usalama wa wapanda baisikeli. Tulikubali kuanza kuongea na chuo cha usafirishaji kuhusu hiyo kwanza.

Ushirika wa kibarua cha baisikeli

Shukuru alitembelea ofisi za wilaya za Kinondoni mara nyingi na mwishoni alionana na Bwana Bukoko ofisa wa ushirika. Alituchanganya, mwanzo alisema NGO tufanye biashara hiyo na baada ya hapo alisema tuanze biashara na tusajili kama ushirika baadaye. Elaine atajaribu kumtembelea kupata taarifa bora.

Ruzuku ya Foundation for Civil Society

Elaine alisahihisha maombi kama wanachama walivyoweka wiki jana. Elaine anafuatalia kupata CV wa walimu kuweka pamoja na maombi.

Video ya usalama wa baiskeli

Hamadi atapata mtu anayemfahamu kutembelea mkutano wetu kuongea kuhusu kufanya nakala za DVD za usalama wa baiskeli.

Juma

Juma bado hajatoa vitu vyake binafsi kutoka ofisi. Atafanya wiki hii.

Mambo ya hela na guta

Filbert alileta Tsh 7,000 ya hela ya guta na bado anadaiwa Tsh 7,000. Edgar aliweka hela inayobaki kutoka mafunzo ya Wamba kwenye benki Tsh 40,000. Juma sasa ana Tsh 7,000 ya hela ya UWABA.